

4.2 UCHANGANUZI WA KARATASI MAHUSUSI

4.2.1 INSHA (102/1)

Jedwali 15: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka ya 2008 – 2011

Mwaka	2008	2009	2010	2011
Alama ya Wastani	14.20	15.40	14.32	16.43
Alama ya Tenganisho	7.18	6.93	6.53	5.61

Jedwali hili laonyesha kwamba kwa kipindi cha miaka hii minne, (2008-2011), matokeo ya karatasi ya kwanza (102/1) yamekuwa yakiyumba, na kwamba watahiniwa wengi hajawaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 40. Katika mwaka wa 2011, matokeo yaliimarika kwa **2.11**. Aidha karatasi hii hajaweweza kuwatenga vyema wanafunzi kulingana na uwezo wao. Alama tenganisho imekuwa ikiyumba kila mwaka.

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

1 Insha ya lazima.

Wewe kama mwanafunzi umepata nafasi ya kumhoji Mkurugenzi wa Habari nchini kuhusu umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Andika mahojiano hayo.

Swali hili lilitihitaji mtahiniwa kuandika mahojiano. Watahiniwa wengi walikosa alama kwa kubadilisha nafasi za wahusika:: Mhoji na Mhojiwa. Wengine walishindwa kuikuza mada kwa kukosa kuimarisha mchakato wenyewe wa mahojiano, na kutokuwa na ujuzi mpana wa umuhimu wa magazeti.

4.2.1 Ushauri kwa walimu

Walimu wawatayarische wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi, kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Elimu.

4.3 MAPENDEKEZO

- 4.3.1 Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.
- 4.3.2 Walimu watumie silabasi za K.I.E na K.N.E.C katika ufundishaji wao.
- 4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa mapana (magazeti, majarida na vitabu katika nyanja anuwai) ili kujifahamisha kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa.Hili litakuza ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala nyeti/masuala ibuka iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.
- 4.3.4 Wanafunzi wahamasishwe kufasiri maswali kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.